

# MAJI NA ROHO - ZAB 103

59

Ubatizo wa Yesu Kristu - mwaka C  
Zab 103, 1-3a,3bc-4, 24ac-25,27-28,29-30

Musique : Toni Iragi K

726

F F6 Am F Em Dm Dm7 F

Ma-ji na ro - ho wa-na-ku-shu - hu - di - a,

728

Dm Gm7 Em Am Bb C Dm

we - we Bwa - na wa u-tu-ku - fu.

730

F Gm A Dm F C Gm Bb C F Em Dm

1. Umevaa utukufu na ungaro,  
umejivika mwanga kama vazi!  
umetandaza anga kama hema,  
juu ya maji umejenga makao yako.
2. Unafanya mawingu kuwa gari lako  
unakwenda juu ya mabawa ya upepo.  
Unafanya pepo kuwa wajumbe wako,  
na ndimi za moto kuwa watumishi wako.
3. Ee Bwana, kazi zako ni nyingi sana,  
dunia imejaa viumbe vyako.  
Bahari iko huku, kubwa na pana sana,  
ndimo wanamokwenda bila hesabu/  
wanyama wadogo na wakubwa.
4. Wale wote wakutazamia Wewe,  
uwape chakula wakati wake:  
Wewe unawapa, nao wanakiokota,  
unafungua mkono wako, wanashiba mema.
5. Ukificha uso wako, wanaangamia,  
ukiondoa pumzi ya uzima, wanakufa,  
wanayarudia mavumbi yao.  
Ukipeleka pumzi yako ya uzima, wanaumbwa tena,  
unafanya upya uso wa dunia.